BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Tisa – Tarehe 26 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

173. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Takriban miaka mitatu iliyopita, katika eneo la Dunga kuanzia kambi ya Jeshi la Kujenga Uchumi (J.K.U) hadi eneo la skuli ya msingi na sekondari ya Dunga, kulijaa maji kufuatia mvua zilizonyesha na inasemekana maji pia yalikuwa yanachimbuka chini ya ardhi, hali ambayo haikuwahi kutokea kwa miaka mingi iliyopita.

(a) Je kufurika huko kwa maji kulisababishwa na nini.

(b) Je, Serikali inatoa wito gani kwa wananchi wa maeneo hayo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

114. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Suala la usafi wa mazingira ni kinga bora kwa ustawi wa afya njema kwa wananchi wetu.

(a) Licha ya ahadi za vipindi tofauti kutoka kwa watendaji wa Manispaa, kwa nini bado kunazagaa taka na majaa katika jimbo la Mwanakwerekwe.

(b) Ni ipi ahadi ya kimkakati ya kuondokana na janga hili.

168. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Vitendo vya uasharati na ukahaba vimeenea katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipi kuviondoa vitendo hivyo katika eneo la Gymkana na eneo la karibu ya mkahawa wa Bavuai hapo Maisara.

(b) Je, vitendo hivyo vimeshughulikiwa vipi katika eneo la Amani Mkoa, hasa ikizingatiwa kuwa mabaa na ulevi yamekithiri katika eneo hilo.

(c) Je, hatua zipi zimechukuliwa kuviondosha vitendo hivyo viovu katika maeneo la messi Dunga na messi ya Ubago na maeneo yote ya fukwe za Unguja na Pemba.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

104. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hivi karibuni, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa fursa 500 za ajira kwa wauguzi wa kike, kwenda kufanya kazi nchini Saudi Arabia.

Ni kwa kiasi gani wauguzi wa kike kutoka Zanzibar waliweza kuitumia fursa hiyo.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

2. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwepo na changamoto ya upungufu wa gari kwa ajili ya kazi za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Unguja na Pemba, hali inayopelekea Afisi ya Baraza kuazima gari katika taasisi nyengine za Serikali au kukodi gari za watu binafsi.

(a) Je, Serikali imefikia katika hatua gani ya kuitatua changamoto hii.

(b) Je, hatua hizo zitachukua muda gani kukamilika.

125. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hivi karibuni tumeshuhudia miradi mbali mbali ya kimkakati ikifunguliwa na mengine kuwekewa mawe ya msingi.

Je, ni kwa kiasi gani wakandarasi wazawa wenye uwezo na viwango wameweza kushirikishwa kwenye ujenzi wa miradi hiyo ya kimkakati.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zoezi la upimaji katika maeneo ya kihistoria linasaidia sana kuwaepusha wananchi kuyavamia maeneo hayo.

(a) Je, ni maeneo gani mpaka sasa yanakabiliwa na changamoto hizo.

(b) Je, kwa nini zoezi la kuyapima maeneo ya kihistoria linachukua muda mrefu kukamilika huku baadhi ya maeneo yakiendelea kuvamiwa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

79. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweka ahadi ya ukarabati wa skuli ya Paje kwa kampuni iliyotembelea kijiji hicho.

(a) Je, Wizara yako inaikumbuka ahadi hiyo.

(b) Je, hatua gani zimefikiwa katika ukarabati wa skuli hiyo.

(c) Je, Wizara yako inawaambia nini wananchi wa kijiji cha Paje.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

42. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa siku nyingi sasa, kumekuwa na kuingiliana sana kwa mawimbi ya sauti (audio frequencies) ya ZBC Radio na radio nyengine katika sehemu mbalimbali za Unguja na Pemba.

(a) Je, ni utaratibu upi hutumika katika ugawaji na uhakiki wa mara kwa mara wa mawimbi ya sauti (audio frequencies) ya kila mtoa huduma aliyepewa leseni Zanzibar.

(b) Je, kwa miaka mitano iliyopita (2018/2019 - 2022/23), ni mapato ya kiasi gani yamekusanywa kutokana na kuanzishwa na kuendeshwa kwa mifumo ya radio au TV Zanzibar.

(c) Je, ni kwa kiasi gani sehemu ya mawimbi ya sauti (audio frequencies) iliyokusudiwa kutumika Zanzibar imetumika au kubakia.

111. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi gani maboresho ya maposho na stahiki za wafanyakazi wa ZBC zimekuwa chachu ya mabadiliko ya kiutendaji wa wafanyakazi hao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunashuhudia hivi sasa miti mingi inayokatwa kwa ajili ya kutengenezea samani ni miti ya matunda ikiwemo mishelisheli, mizambarau, miembe, minazi na mengineyo.

Je, ni upi mkakati wa Wizara yako katika kulishughulika tatizo hili ambalo siku za mbele litaliingiza taifa kwenye ukame wa matunda.

**Wizara ya Afya:**

46. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wanafunzi wa shehia ya Maziwani katika jimbo la Pandani wanatoa shukrani kwa Serikali kwa kukiwezesha kituo cha afya Maziwani kuanza kutoa huduma, japo ni baada ya miaka zaidi ya 10 tokea kujengwa kwake. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kutokuwepo kwa makaazi ya daktari au muuguzi kwa ajili ya huduma endelevu na za dharura.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba ya daktari wa kituo cha afya Maziwani.

(b) Je, ni upi mpango wa dharura wa sasa wa kuhakikisha kunapatikana huduma endelevu na za dharura nje ya muda wa kazi.

(c) Je, kwa sasa kituo cha afya cha Maziwani kina wafanyakazi wangapi wenyeji wa shehia ya Maziwani na wangapi wenyeji wa jimbo la Pandani.

51. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo zuri kwamba Serikali hufuatilia utendaji wa wafanyakazi wake na kuwachukulia hatua stahili pale wanapokosea katika utekelezaji na usimamizi wa majukumu yao. Mfano mzuri ni watumishi waliofukuzwa kazi kwa kesi za uzembe katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

Hata hivyo, utekelezaji wa taratibu za kuwaadabisha na kuwachukulia hatua watumishi wa Serikali pale wanapokosea ni jambo la matukio na sio linalotekelezwa kwa kila kosa.

(a) Je, ni hatua zipi za ziada walizochukuliwa watumishi waliofukuzwa kazi mwaka wa 2023 kwa kesi za uzembe katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

(b) Je, kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023), ni watumishi wangapi wa Serikali wamechukuliwa hatua ya kufukuzwa au kusimamishwa kazi na kwa makosa gani.

(c) Je, katika utaratibu mpya wa sasa wa uendeshaji wa Hospitali za Serikali kwa njia ya Ubinafsishaji, ni mamlaka gani itawaadabisha watumishi watakaohusishwa na kesi za uzembe.

<u>**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**</u>

77. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Jimbo la Paje ni eneo lenye shughuli za utalii kwa asilimia kubwa, lakini bado linakabiliwa na changamoto kubwa ya ubovu wa barabara inayotoka Kitogani hadi Paje.

(a) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa na ujenzi huo utachukua muda gani, ili kupunguza uharibifu wa magari yanayopita katika njia hiyo.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa jimbo la Paje.

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe tunampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa maendeleo makubwa sana aliyoyafanya ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe.

Je, ni lini baadhi ya njia za ndani ikiwemo Kidatu hadi kwa Mwarabu kuelekea Ubaya Ubaya, itafanyiwa matengenezo ili kuwaondolea wananchi usumbufu mkubwa wanaoupata.

181. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na juhudi kubwa za kujenga barabara za ndani tena kwa teknonojia ya kisasa kabisa, kuna uwezekano mkubwa wa kutokea kwa mafuriko katika majumba ya wananchi waliopitiwa na barabara hizo, hususan katika maeneo ya Mwanakwerekwe, Kwa Mchina na Mombasa.

(a) Je, Wizara yako imefanya tathmini yoyote ya kujua majanga yatakayotokezea baada ya ujenzi wa barabara hizo za ndani, hasa katika maeneo ya Mombasa.

(b) Je, hatua gani zitakazochukuliwa ili kuzuia majanga yanayofikiriwa kutokezea.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**26 Februari, 2024.** **KATIBU WA BARAZA.**